



COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD

Tuesday, 26th November, 2024

Third Assembly – Third Session
EIGHTY EIGHTH SITTING

*[The County Assembly met at 11:19a.m at the County Assembly Buildings]
[The Speaker (Honourable Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]*

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Clerk, next order, please.

PAPER

REPORT ON THE REVIEW OF THE MOMBASA NI YANGU PROGRAMME

Yes, Honourable Jacktone Madialo. Please lay the Paper.

Hon. Madialo: Thank you Mr. Speaker, Sir. I wish to lay the Paper on the Report on the review of the *Mombasa Ni yangu* Programme.

[Paper laid]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much, Honourable Jacktone. Thank you, Madialo. Yes, Clerk, next order, please.

MOTION

ADJOURNMENT OF THE COUNTY ASSEMBLY

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, Leader of the Majority party. Please move the Motion.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker, Sir, I beg to move the following Motion.

That pursuant to provision of Assembly Standing Orders 30, subsection (1), this County Assembly adjourns today, Tuesday, and resume next week, Tuesday, 3rd, December, 2024.

May I, ask Honourable Eliud Kimari to second the Motion.

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 1*

Hon. Kimari: Thank you, Mr. Speaker, I second.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Honourable Members, I now propose the question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on adjournment of the County Assembly to be considered by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question proposed and agreed to]

[Question put and agreed to]

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, Leader of the Majority party, please make your contributions.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, niwaombe tu Waheshimiwa kwa kuafiki ya kwamba tutatize kalenda yetu ya wiki hii kwa sababu makhsusi Mheshimiwa Spika. Kuna ratiba iliyoratibiwa ya masuala ya chama ambayo Mheshimiwa Spika takriban Waheshimiwa ishirini na sita katika Bunge hili ni wanachama wa chama cha chungwa na wote wanastahiki kuhusika katika uchaguzi wa chama ilioratibiwa kesho. Mheshimiwa Spika, na mipango hii inanzia leo mchana hivyo basi kwa kuhofia kutokua na idadi kamili inayostahiki kwa shughuli za Bunge kuendelea kwa sababu watakua wamesalia, Waheshimiwa sita wa chama cha UDA, na ambao hawawezi kuendesha shughuli za Bunge, niombe ridhaa ya Bunge hili Waheshimiwa waweze kuafiki ili tuweze kushiriki katika zoezi hili la kikatiba kwa mujibu wa sheria za vyama katika nchi yetu ya Kenya na turudi katika kuendelea shughuli za Bunge. Juma lijalo siku ya Jumanne Mheshimiwa Spika tarehe 3 December na sisi Waheshimiwa tuweze kwenda kwa zoezi hili kuhamasisha wananchi wanao shiriki lakini zaidi tuwasisitize wananchi wetu. Kwa kutekeleza suala hili kwa utulivu na amani tukizingatia kwamba shule zimefungwa vijana wetu mitaani wakipata fursa ya vurugu huenda wakachangia pakubwa uvunjifu wa usalama katika maeneo yetu, ahsante Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Kai. Please make your contributions.

Hon. Kai: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii, lakini nauliza kama Kiongozi wa Wengi ni sawa kusema kwamba wanachama wa UDA hawana uwezo wa kuendesha Bunge, tunazungumzia idadi ama ni uwezo manake sisi tumekuja hapa na tuna uwezo mkubwa na tuna elewa jinsi Bunge linavyoendesha.

The Speaker (Hon. Khatri): Kwa hivyo Mheshimiwa Kai ni point of information ama...

Hon. Kai: *[Off microphone]*.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Majority Leader.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kai, labda nitumie lugha anayo ifahamu yeye zaidi ya kwamba kwa shughuli za Bunge kuendelea lazima kuwe na angalau wanachama wa Bunge hili angalau kumi na tatu, idadi wao UDA ambao kesho wako uhuru kuendelea na shughuli wako sita. Kwa hivyo ki idadi hawana uwezo wa kuendesha shughuli kwa siku ya kesho.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Prischilla, please make your contributions.

Hon. Mumba: Ahsante Mheshimiwa Spika. Mimi nasimama kuunga mkono kikamilifu hoja iliyoletwa na Kiongozi wa Wengi, kwa sababu ni ukweli kama alivyo nukuu Nyumba hii imebebwa na chama chetu cha ODM na sote tutakua tuko nyanjani tukiunga mkono na tukifanya siasa yetu ya chama. Maana ikiwa chama ndio kimekuleta lazima pia kama chama kinataka kufanya kura zake ni lazima pia na sisi tuingize vichwa vyetu pale na tujue siasa ya chama inaendeshwa vipi na ninashukuru Mungu sana kwa sababu katika chama changu hapa tuko wingi wingi kwa chama. Kwa hivyo kesho ikiwa tumefunga Bunge mpaka Jumanne, sioni kukiwa na tatizo na ikiwa wenzetu wanataka kuendelea waendele, lakini kama ninavyojua mimi hapa namba hakuna ya kuendeleza hili jumba. Kwa hivyo hatuna budi kulifunga hili Bunge mpaka Jumanne kwa sababu hata mukaja wenzetu hiyo namba mutaitoa wapi? Pengine mlete wengine wa kutoka mbinguni washuke. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Prischillah. Yes, Honourable Frankline Makanga.

Hon. Makanga: We koma!

[Laughter]

The Speaker (Hon. Khatri): Order! order! Honourable Members.

Hon. Makanga: Mheshimiwa Spika, naomba unilinde na hawa watu wa UDA kwa sababu kile wanakosa kujua ni kwamba mimi ni mwana wa ODM na yale ninayo yasema nayasema nikiwa mwana ODM ila labda Kiranja wa Bunge kulingana na Mswada ulioko imesema tunaahirisha Bunge hadi kesho, na yeye amesema hadi Jumanne. Sasa nafikiri hapo itabidi tuwekwe wazi tujue Bunge linaghairishwa vipi Novemba 27th Jumatano! Kwa hivyo Mswada mbele yetu uko na makosa labda utatungoza tujue vile tutafanya lakini mimi naunga mkono ya kwamba Bunge liweze kuahirishwa ili turudi mashinani kutengeza chama chetu tukipendacho. Hata hawa wa UDA Mheshimiwa Spika, nazungumza nao hapa wote wako tayari kuja ODM kwa hivyo kazi kwako! Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you, Honourable Franklin. Yes, Honourable Leyla Nyache, please make your contribution.

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia. Kwanza nimemuunga mkono Kiongozi wa Wengi katika Bunge hili Mheshimiwa Mwamwiri kwa kuweza kuleta hoja hii. Kuna msemu Mheshimiwa Spika wengi wape, kwa hivyo mimi nawaomba ndugu zangu wa UDA tukubaliane tu kwa uzuri tushirikiane na tuingie mashinani kwende tukakuze chama chetu. Sisi sote ambao tuko wengi hapa tumechaguliwa na ODM na shughuli za ODM mpaka tuingilie kati, tujue na sisi tuko upande gani, hivyo basi tusipoenda kwa wananchi wetu wasipotuona pale ile ODM haitaonekana manake ODM ni sisi na sisi ndio ODM. Kwa hivyo mimi nimesimama kuunga mkono na kuwaambia ndugu zangu wa UDA tushirikiane maadamu muko wachache tushirikianeni katika chama chetu cha ODM na nyinyi wenyewe mutaona natija katika hicho chama, ahsanteni sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you, ahsante Mheshimiwa. Yes, Honourable Athman Mwamwiri, you may reply to the Motion.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Niwashukuru Waheshimiwa wenza kwa kuweza kuunga mkono hoja hii na pia nishukuru wale ndugu zangu wanachama wa chama cha UDA ambao wamejikubali kwa uchache wao na kuafiki kwa wingi wetu ya kwamba tuweze kuahirisha vikao hivi mpaka juma lijalo Mheshimiwa Spika. Cha kuisitiza tu Mheshimiwa Spika ni kwa Waheshimiwa wenza ambao watakua nyanjani katika zoezi hili tuhakikishe tumedumisha amani kwa sababu utulivu wa mitaa yetu ndio fursa ya maendeleo na uwekezaji katika maeneo yetu. Ahsante Mheshimiwa Spika na kila la heri kwa Waheshimiwa na wale ambao wanagombania viti katika vituo vyao pia kila la heri. Shukran.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much, Honourable Athman Mwamwiri, Leader of majority party. Honourable Members, I now put the question that the Motion by the Honourable Athman Mwamwiri on adjournment of the County Assembly be approved by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question put and agreed to]

So, the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on adjournment of the County Assembly is adopted by the House. Yes, Clerk, next order, please.

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Tuesday, 3rd December, 2024 at 10:00a.m.

The House rose at 11:30a.m.